BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA WA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Nane – Tarehe 30 Septemba, 2016.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Ushahidi Sura ya Tano na Kuandika Sheria Mpya ya Ushahidi na Mambo Mengine Yanayohusiana Nayo.

Waziri wa Fedha na Mipango:

Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Nam. 2 ya 2005, kuweka masharti bora zaidi kwa ajili ya ufanisi na usimamizi imara wa Mfuko na Mambo yanayohusiana na Hayo.

Mswada wa Sheria ya Kutunga Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma na Kuweka masharti Bora ya kudhibiti na Kusimamia Fedha za Umma na Kuweka Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo na Kufuta Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Serikali Nam. 12 ya 2005.

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Manunuzi na Uuzaji wa Mali za Serikali Nam. 9 ya mwaka 2005 na Kutungwa Sheria inayoanzisha Mamlaka ya Manunuzi na Uuzaji Mali za Umma na Kuweka Masharti Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub:

Maombi ya Wananchi (Petition) kuhusu Kuchukuliwa hatua za haraka za Kuepusha Usumbufu usiokuwa wa lazima wa kupatikana kwa huduma mbali mbali za Afya katika Hospital ya Mnazi Mmoja.

Mheshimiwa Mohammed Said Mohamed (Dimwa):

Hoja ya Mjumbe kuhusu ukiukwaji wa Sheria kwa baadhi ya Taasisi ambazo zinatakiwa kuwasilisha taarifa zake mbele ya Baraza la Wawakilishi kwa mujibu wa Sheria.

II. MASWALI:

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:

180. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais:

Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ndio yenye dhamana katika chombo hichi cha wananchi katika kusimamia uwajibikaji wa Mawaziri na Naibu Mawaziri.

Mhe. Rais wa Zanzibar katika kipindi kilichopita aliagiza Mawaziri kujibu kwa kina masuala wanayoulizwa na kama hawana jawabu wachukue muda wa kujibu kwa maandishi.

Je, ni lini mawaziri na Manaibu Mawaziri watafanyiwa semina kuelekezwa namna ya kujibu maswali kama alivyoagiza Mhe. Rais hasa kwa kuwa masuala yanayoulizwa yamezingatia maslahi ya Zanzibar na wananchi wake kutokana na umuhimu wake.

Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

6. MHESHIMIWA MWANTATU MBARAKA KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Kwa kuwa Sura ya 3 ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kifungu cha 12(1) kinasema kuwa watu wote ni sawa mbele ya Sheria na wanayo haki ya kutokubaguliwa na kulindwa. Na kwa kuwa miongoni mwa haki za msingi za binaadamu ni kufanya kazi na kupata ujira ambayo imeelezwa katika kifungu cha 21(3).

Kutokana na maelezo ya vifungu hivyo vya Katiba Serikali imejipanga vipi kuona kuwa Watu Wenye Ulemevu wenye sifa wanafaidika na haki zao hizo za Kikatiba.

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

190. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi amesema vijana wanaofanya biashara mitaani hawastahili kubugudhiwa ili wapate riziki na kufanikisha utekelezaji wa ilani ya CCM ya vijana kujiajiri ili kuondokana na umasikini.

a) Je, Zanzibar tumejifundisha nini juu ya uamuzi wa Rais John Pombe Magufuli kwa kuwajengea wafanyabiashara wadogo wadogo (machinga) eneo la Kariakoo kuendelea na biashara zao bila ya kubugudhiwa.

b) Je, ni lini Serikali itaachia wafanye biashara zao katika maeneo ya Darajani, Mchangani na maeneo ya katikati ya Mji Mkongwe.

c) Je, hatua ya kuwakamata wafanyabiashara wadogo wadogo wakiwemo wauza kahawa, mikate, njugu, machungwa, magazeti inawasaidia kupunguza umasikini au kuzidisha umasikini na uhalifu.

159. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Eneo la kuzikia (makaburi) la Mwanakwerekwe kwa miaka mingi limekuwa likitumika kuzika wafu na hadi kufikiriwa kuwa limeshajaa. Hivi sasa kumekuwa na mtindo wa kuyajengea makaburi hayo na kupelekea nafasi ya kuzikia kuzidi kuwa ndogo.

a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka alama za kudumu katika makaburi hayo, ambazo zitachukuwa nafasi ndogo kuliko ilivyo hivi sasa.

b) Kwa kuwa eneo la Mwanakwerekwe limeshaonekana kujaa na nafasi iliyobakia kuwa ni ndogo sana, Je, Serikali imeshatafuta eneo jengine la kuzikia na kulifunga eneo la Mwanakwerekwe.

c) Hatua gani zinachukuliwa kudhibiti vitendo vya uharibifu wa mazingira ya eneo la makaburi ya Mwanakwerekwe.

Wizara ya Fedha na Mipango:

66. MHESHIMIWA MIHAYO JUMA N'HUNGA (Jimbo la Mwera)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Kwa kuwa Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) imekuwa na wateja wengi wanaotumia Benki hiyo wakiwemo Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Watumishi wa Baraza. Na kwa kuwa huduma ya kutumia mashine ya ATM inarahisisha sana, huduma za Benki na haitumii muda mwingi.

Je, Wizara yako ina mpango gani kuanzisha huduma hii katika eneo la Baraza la Wawakilishi, Chukwani na lini itaanzishwa.

Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:

22. MHESHIMIWA MTUMWA PEYA YUSSUF (Jimbo la Bumbwini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:

Usambazaji wa huduma ya umeme vijijini ni uamuzi mwema wa Serikali ya Mapinduzi, Zanzibar ili kuwawezesha wananchi katika maeneo hayo kuendesha shughuli zao kwa ufanisi zaidi. Katika Jimbo la Bumbwini kulikuwa na mradi wa usambazaji umeme kutoka Zingwezingwe kwenda Pangatupu. Hata hivyo, mradi huu umekwama kwa muda mrefu sasa.

a) Ni sababu gani zilizopelekea mradi huu kukwama.

b) Je, ni lini huduma hiyo ya umeme itasambazwa hadi kufikia katika kijiji cha Pangatupu kilicho katika shehia ya Kidanzini ili wananchi wa kijiji hicho waweze kufaidika na huduma hiyo muhimu

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

175. MHESHIMIWA. ALI SULEIMAN ALI (Jimbo la Kijitoupele)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

Hali ya ukataji wa minazi katika kisiwa cha Unguja ni mbaya sana, pamoja na jitihada zinazofanywa na Wizara kupitia Idara husika.

Kwa kuwa minazi inakatwa, na kupelekwa katika viwanda mbali mbali Unguja. Je, Mhe. Waziri ni hatua gani madhubuti zilizoandaliwa juu ya kukomesha tatizo hili.

Wizara ya Elimu na Mafunzo na Amali:

143. MHESHIMIWA. NASSOR SALIM ALI (Jimbo la Kikwajuni)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na mafunzo ya Amali

Kwa kuwa uanzishwaji Tume ya Utumishi ya walimu ni miongoni mwa Mapendekezo ya mashirika ya Umoja wa Mataifa ya UNESCO na ILO yanayozitaka nchi wanachama kuhakikisha zinaunda Tume hizo katika nchi zao.

a) Je, Wizara haioni kwamba ipo haja ya kuanzishwa kwa Tume ya Utumishi ya Walimu

b) Je, Sera ya elimu ya Zanzibar ya mwaka 2006 inasema nini kuhusu suala la walimu kuwa na chombo hicho cha kusimamia ajira ya walimu hao.

c) Je, Wizara imefanya mchakato gani wa kuandaa mapendekezo ya kuundwa Tume hiyo hapa Zanzibar.

Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:

148 MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:

ZBC ni chombo cha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kinachotoa habari za ukweli na uhakika lakini inaonekana haina nguvu ya kurusha matangazo kwa Zanzibar na Tanzania yote kwa jumla.

a) Je, Serikali ni lini italiondoa tatizo hilo.

b) Je, Serikali imejipangaje, kuwasomesha na kuwaongezea uzoefu na ufanisi watangazaji wake na kuimarisha miundombinu ya mitambo yake.

c) Kwa nini waandishi wa ZBC hasa katika kisiwa cha Pemba hawaonekani kutafuta habari na kuingia katika ushindani na waandishi wengine.

Wizara ya Afya:

58. MHESHIMIWA SULEIMAN MAKAME ALI (Jimbo la Ziwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya

Kwa kuwa suala la Afya ni jambo la msingi kwa kila binaadamu. Na kwa kuwa bila ya kuwepo huduma za afya zilizobora maisha ya binaadamu yatakuwa hatarini. Na kwa kuwa kumekuwepo na jitihada za kujenga vituo vya afya ili kuwafikishia wananchi huduma hizo, katika maeneo mbali mbali ya nchi yetu.

Je, ni kwa nini mpaka hivi sasa kituo cha Afya Birikau hakijamaliza kujengwa.

III. MAOMBI (PETITIONS)

Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub:

Maombi ya Wananchi (Petition) kuhusu Kuchukuliwa hatua za haraka za Kuepusha Usumbufu usiokuwa wa lazima wa kupatikana kwa huduma mbali mbali za Afya katika Hospital ya Mnazi Mmoja.

IV. HOJA YA MJUMBE:

`Mheshimiwa Mohamed Said Mohamed:

Hoja ya Mjumbe kuhusu ukiukwaji wa Sheria kwa baadhi ya Taasisi ambazo zinatakiwa kuwasilisha taarifa zake mbele ya Baraza la Wawakilishi kwa mujibu wa Sheria.

V. HOJA ZA SERIKALI:

Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Ushahidi Sura ya Tano na Kuandika Sheria Mpya ya Ushahidi na Mambo Mengine Yanayohusiana Nayo – Kusomwa kwa mara ya Kwanza.

Waziri wa Fedha na Mipango:

Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Nam. 2 ya 2005, kuweka masharti bora zaidi kwa ajili ya ufanisi na usimamizi imara wa Mfuko na Mambo Yanayohusiana na Hayo – Kusomwa kwa mara ya Kwanza.

Mswada wa Sheria ya kutunga Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma na Kuweka masharti Bora ya kudhibiti na Kusimamia Fedha za Umma na Kuweka Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo na Kufuta Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Serikali Nam. 12 ya 2005 – Kusomwa kwa mara ya Kwanza.

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Manunuzi na Uuzaji wa Mali za Serikali Nam. 9 ya mwaka 2005 na Kutungwa Sheria inayoanzisha Mamlaka ya Manunuzi na Uuzaji Mali za Umma na Kuweka Masharti Mengine Yanayohusiana na Hayo – Kusomwa kwa mara ya Kwanza.

Zanzibar, **(Amour M. Amour)**
30 Septemba, 2016. **KNY. KATIBU WA BARAZA.**